# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# OFISI YA WAZIRI MKUU - TAMISEMI

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA KILIMANJARO KATIKA WILAYA YA SIHA 2026

.

**OFISI YA WAZIRI MKUU - TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA SIHA**
**SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA KILIMANJARO**

**Namba za simu:**
**1.Mkuu wa shule:0754 026 793**
**2.M/mkuu wa shule:0762 210 963**
**3.Mwandamizi Taaluma:0763 355 523**

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi …………………………
…………………………………………………………..
S.L.P ………………………………………………….
…………………………………………………………..

**YAH: <u>MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA KILIMANJARO KIDATO CHA KWANZA 2026.</u>**

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Kwanza katika Shule ya Sekondari ya Wasichana Kilimanjaro mwaka **2026**.Shule hii ipo umbali wa kilomita kumi (12) kutoka mji wa Sanya Juu, Wilaya ya Siha Mkoani Kilimanjaro.Kwa wanaotokea Moshi mjini au Arusha watashukia Standi ya Boma Ng´ombe na kupanda gari ya Sanya Juu na kushuka mwisho wa gari kisha atachukua usafiri wa kuja Shuleni, Mwanafunzi anatakiwa kuripoti Shuleni tarehe ……………………. mwisho wa kuripoti ni tarehe………………**Mwanafunzi akichelewa ndani ya kipindi hicho nafasi yake itajazwa na mwanafunzi mwingine.**

**MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:**
**Sare za Shule;**

1. Sare ya shule hii ni sketi mbili (2), rangi ya **"KIJANI KIBICHI"** suit material, (kitambaa kizito) mshono wa rinda box mbele na nyuma yenye "belt dogo" NDEFU HADI KWENYE KIFUNDO CHA MGUU CHINI KABISA (ZINGATIA MAELEZO HAYA).
2. Mashati mawili (2) meupe yenye mikono mifupi aina ya" **TOMATO".**
3. Wanafunzi wa Dini ya Kiislam waje na Shungi ya rangi nyeupe mbili kwa ajili ya darasani na kwa ajili ya kuvalia nguo za kushindia, shungi isifunike viganja vya mikono na zisiwe na urembo wowote.
4. Sare ya Michezo ni truck suit rangi ya "**kijivu**" yenye mistari myeupe pembeni isiyobana. Koti la 'tracksuit' isiwe na kofia.
5. Viatu vya shule ni vyeusi vya ngozi vya kufunga na Kamba kuanzia matundu manne hadi sita (sio buti) visiwe na kisigino, (visiwe aina ya **facebook**) na raba nyeusi za michezo.

6. Soksi nyeupe za kutosha ndefu, ‘simple shoes’ nyeusi za kufunika (jozi moja), kandambili jozi moja (asije na yeboyebo), khanga, gauni la kulalia na taulo.
7. ” Pull – neck” nyeusi au nyeupe
8. Aje na magauni mawili marefu yanayovuka magoti ya rangi ya “**kijani draft”** (kijani kibichi) (mshono wa solo) yenye mikono mifupi na kola “baby colar”colar ifanane na kitambaa cha gauni siyo nyeupe, na suruali yake kama nguo za hushindia. **Nguo nyingine haziruhusiwi**.
9. ‘T- shirt’ moja rangi ya **kijivu** yenye kola (form six).isiyo na maandishi,mistari wala alama yoyote aina ya (**180 type ash grey)**
10. Madaftari ‘counter book 3 Q’ yasiyopungua kumi (10).
11. Ream 2 moja (01) ya karatasi aina ya ‘Rotatrim/double A/Top copie/NO1: kwaajili ya kuchapa na rulled ( yenye mistari kwa ajili ya kujibia mitihani.
12. Vitabu vya masomo kutoka TIE (Tanzania Institute of Education) Mtaala mpya.
13. Faili (flat plastic file) dogo la kutunza kumbukumbu za mwanafunzi.
14. 1 “mathematical set”, rula ndefu, kalamu za wino za kuandikia, penseli, kifutio, “stapler machine”, “graph pad”kamusi (English/Swahili au English/English). Kila mwanafunzi anatakiwa awe na kamusi yake, saa ya mkononi kwaajili ya kutunza muda.
15. Godoro saizi **"futi 2.5"**
16. Shuka za kulalia mbili (02), blanketi la kawaida,rangi yoyote ‘student size’, mto , chandarua nyeupe ya duara au mstatili na ‘bed cover’( shuka la kutandika juu ya kitanda mbili (02) ya rangi ya ‘pink’pamoja na foronya zake ili kuleta ufanano).
17. Nguo za ndani za kutosha.Asije na ‘boxer’.
18. Vyombo vya chakula,sahani, kijiko na kikombe (viwe vya bati aluminium) **vya plastic haviruhusiwi**.
19. Ndoo moja (01) ya kuchotea maji yenye ujazo wa lita 10 kwa matumizi yake binafsi na ndoo moja (01) yenye ujazo wa lita 10 kwa ajili ya matumizi ya shule (yenye rangi ya kijani ‘green’)
20. Kila mwanafunzi aje na fagio la kutolea buibui. Tafadhali zingatia ubora
21. Slasher (fyekeo) lililonolewa.
22. Mopper na ndoo yake.
23. Sabuni ya Maji lt.5.aina ya Dexi.
24. Sanduku dogo (saizi ya kati) la bati la kuwekea nguo zake na kufuli lake imara. Asije na sanduku lenye material ya nguo/ngozi” Suit case” hatutalipokea. **Asije na begi lenye**” **Charge”**

**(USB BAG) saa" electronic watch" au kifaa chochote cha 'electronics' kinachohitaji kutumia umeme.**

25. Jembe lililonolewa na mpini wake.
26. Brush ngumu (zingatia ubora).
27. Sweta 'V' – shape shingoni ya rangi ya **KIJANI KIBICHI** mbili (2**),**
28. Aje na kofia ya kijani kibichi(boshori) isiyo na maandishi wala urembo wowote.
29. Begi dogo la mgongoni kwaajili ya kubebea madaftari na vitabu.

**NB.** ***KILA MWANAFUNZI AWEKE ALAMA YA MAJINA YAKE MATATU KATIKA VIFAA VYAKE VYOTE SIO HERUFI.***

### 1.1 Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 1.2 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku(Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;

x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari;na

xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**1.2 MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE NI PAMOJA NA:**

i. Wizi;

ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;

iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;

iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;

v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;

vi. Ni marufuku mwanafunzi kusuka nywele. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.

vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya.

viii. Uvutaji wa sigara.

ix. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;

x. Kupata ujauzito au kutoa mimba;

xi. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;

xii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;

xiii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;

xiv. Kudharau Bendera ya Taifa;

xv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na

xvi. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**MUHIMU:**

i. Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;

ii. Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;

iii. Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa kibali maalum kutokana na tatizo litakalokuwa na uzito mkubwa kama kufiwa na mzazi/mlezi anayemlea,au ugonjwa wa mwanafunzi

unaothibitika kuwa shule inahitaji mzazi asimamie kwa karibu matibabu ya mwanafunzi.Aidha taarifa ya msiba itolewe kiofisi kwa kufuata Sheria,Kanuni na Taratibu za Kiserikali.

iv. Mwanafunzi haruhusiwi kuja na manukato ya aina yoyote, mfano mafuta yenye harufu kali,deodorant, spray ,shower gel n.k.

v. Mwanafunzi haruhusiwi kuja na cream ya aina yoyote.

vi. Mwanafunzi atapokelewa Shuleni akiwa amevaa sare ya Shule na si vinginevyo.

**NYARAKA MUHIMU ZA KUJA NAZO SHULENI**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na

ii. Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali / imeambatanishwa (**kiambatanisho A)**

iii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi imeambatanishwa **(kiambatanisho B)**

**iv.** Fomu ya mzazi na mwanafunzi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule /imeambatanishwa; **(kiambatanisho C)** mwanafunzi ahakikishe anaye soma sharia zote akiwa na mzazi wake.

v. Picha moja (2) ya mwanafunzi kwaajili ya file (passport size) iliyopigwa hivi karibuni (kwa shati jeupe).

vi. Form **D:** Ahadi ya mzazi/mlezi.

vii. Form **E** form ya usajili.

viii. Vii.Nakala ya cheti cha kuzaliwa.

## 2.0 MENGINEYO KWA UMUHIMU

i. Wazazi/walezi hawaruhusiwi kutembelea wanafunzi wawapo shuleni isipokuwa kwa ratiba maalum itakayopangwa na shule. Hii itawasaidia kutumia muda wao vizuri zaidi katika kujisomea.

ii. Ni vyema mzazi ukahakikisha mtoto anapokuja shuleni amechukua tahadhari zote za kiafya ikiwemo Mwanafunzi kuwa na Bima ya afya ya NHIF na nyinginezo kwa ambao hawatakuwa nazo waje na fedha Tshs 50,400/= kwa ajili ya Bima ya afya ya NHIF

**iii.** Shule itawapa wanafunzi chakula bora na cha kutosha hivyo mwanafunzi **haruhusiwi** kuja shuleni na chakula cha aina yoyote hivyo, kila mwanafunzi anatakiwa aridhike na chakula cha shule. **HAKUNA CHAKULA MAALUM (SPECIAL DIET).**

iv. Ni wazi kuwa mwanafunzi lazima apewe pesa za matumizi na ni wajibu wa mzazi/mlezi kumpa binti yake kiasi cha pesa kwa ajili ya matumizi madogo madogo kama vile, sabuni kalamu, nk sio busara kumpa mtoto pesa nyingi kwani hii husababisha wizi, mashindano, ubaguzi, tabaka, ugomvi na urafiki usiokuwa na msingi.

Kutokana na baadhi ya changamoto zilizojitokeza kuhusu fedha za matumizi zinazotumwa kwa wanafunzi ikiwemo kuibiana wakiwa bwenini, mzazi/mlezi kutuma fedha kwa mwalimu bila kutoa taarifa ya jina la mwanafunzi na kusababisha mwanafunzi kutopokea fedha zake kwa wakati, au mzazi kutoa taarifa kuwa alituma pesa kupitia wakala kwa mwalimu na kumbe fedha hazikutumwa. Hivyo, Uongozi wa Shule unashauri umfungulie mwanao akaunti katika benk mojawapo za **NMB, CRDB au UCHUMI** au aje na shilingi **10,000/=** kwa ajili ya kufungua akaunti hiyo ambapo utakuwa unaitumia kutuma fedha ya matumizi na wakala wa benk hizo wanafika shuleni kwa ratiba iliyopangwa na shule ili wanafunzi kuweza kutoa fedha zao.

**v. Siku za mapumziko( jumamosi, jumapili na sikukuu ) wanafunzi watapokelewa kuanzia saa 4:00 asubuhi hadi saa 10:00 jioni kila mzazi/mlezi azingatie hili ili kuondoa usumbufu.**

**vi.** Shule ina utaratibu wa kuwa na vikao vya wazazi mara moja kwa mwaka, hivyo kwa mwaka huu kikao kitafanyika tarehe **07/3/2026**.

**vii.** Mzazi anatakiwa kumsafirisha binti yake wakati wa kuja shule na anaporudi nyumbani wakati wa likizo. Ni muhimu fedha za usafiri zitumwe mapema mara baada ya kupokea taarifa wakati utakapofika ili usafiri wa pamoja upangwe na shule

***viii.*** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa.** ***TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE. NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZILIZOPO KATIKA FORM HII:***


**ix.** Mara upatapo fomu hii unaweza kutuma ujumbe wa kuomba kuungwa kwenye group la wazazi la whatsap kwa namba **0762 210963** ni **muhimu.**

**HITIMISHO:**

Wazazi tunaomba sana tuwe na malezi ya pamoja ili watoto waendelee na wapate kile walichokifuata shuleni, yaani **ELIMU.** Msisisitizo wa Bodi ya Shule ni kwamba kila mwanafunzi anatakiwa kusoma kwa bidii na kufaulu kwa kiwango cha asilimia **80%** au zaidi katika kila somo. Sheria zote hizo zinalenga kumfanya mtoto apate mazingira bora ya kujisomea na hatimaye aweze kufaulu vizuri masoma yake.

***NB. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.***


***KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA KILIMANJARO***



…...............................

**MARIANA D. MSANGI**

**MKUU WA SHULE**




**FORM A**

**SIHA DISTRICT COUNCIL KILIMANJARO GIRLS SECONDARY SCHOOL**

## MEDICAL EXAMINATION FORM

To be completed by medical Officer in respect of all form entrants.

a. Full Name……………………………………………………………………………………………….
b. Age…………………………………………………………………………………………………….
c. Blood count (Red and White) ……………………………………………………………………..
d. Stool Examination………………………………………………………………………………...
e. Urine analysis ……………………………………………………………………………………..
f. Syphilis test ……………………………………………………………………………………….
g. T.B. Test ………………………………………………………………………………………….
h. Eye Test …………………………………………………………………………….............
i. Ears ………………………………………………………………………………………………
j. Chest ……………………………………………………………………………………………….
k. Spleen ……………………………………………………………………………………………...
l. Abdomen ………………………………………………………………………………………….
m. ADDITION INFORMATION: e.g. physical or chronic family diseases
etc. ……………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………
……
……………………………………………………………………………………………………….

I certify that the above is fit to pursue studies

Signature…………………………………. Designation …………………….

Section……………………………………. Date……………………………

STUDENT: You must bring this completed form when you come to School. No student will be allowed to enroll without certificate of physical fitness.

**FORM B**

**OFISI YA WAZIRI MKUU -TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA SIHA**

**SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA KIMANJARO**

# HATI YA UTII WA SHERIA

Mimi, Bwana/Bibi …………………………………………………………………… Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi ……………………………………………….. nimesoma kwa makini Sheria za Shule kama zilivyoandikwa katika maagizo kwa wazazi/walezi, nimekubali na nitashirikiana na Shule kuona kuwa mwanangu anazingatia sheria zote kwa manufaa ya Umma.

Mimi …………………………………..Binti wa Bwana / Bibi ……………………………………………. nimesoma kwa makini Sheria za Shule kama zilivyoandikwa na nimekubali. Naahidi kuwa nitazifuata na kuzitii nikijua kuwa naelimishwa na Umma kwa manufaa ya Umma.

…………………………………………….. ………………………………………..

SAINI YA MWANAFUNZI SAINI YA MZAZI

**FORM C**
**SIHA DISTRICT COUNCIL**
**KILIMANJARO GIRLS SECONDARY SCHOOL**

**STUDENT INFORMATION SHEET: -**

(This form is to be completed by form five and student transferred to the school. Parts A, B and C to be completed by the student)

**A: PERSONAL PARTICULARS:**

NAME: …………………………………………………………………………………………………………………………

DATE OF BIRTH: ……………………………………………………………………………TRIBE: ……………………………………. …..

RELIGION: ………………………………………………………………………… DENOMINATION……………………………….

FATHER'S NAME: ………………………………………………………………… OCCUPATION………………………………………..

MOTHER'S NAME: ……………………………………………………………… OCCUPATION ………………………………………..

GUARDIAN'S NAME: ……………………………………………………………… OCCUPATION ………………………………………..

NUMBER OF SISTER'S: ………………………………………………………… NUMBER OF BROTHERS ………………………

FATHER'S TELEPHONE NUMBER: ……………………………………… MOTHER'S TELEPHONE NO ……………………

HOME ADDRESS: …………………………………………………………………………………………………………………..

ANY PHYISICAL/ MEDICAL DISABILITY ………………………………………………………………………………………

**B: PRIMARY EDUCATION (IF ANY): -**

…………………………………………… PRIMARY SCHOOL: FROM………………………… TO ………………………

…………………………………………… PRIMARY SCHOOL: FROM …………………………….

TO ……………………… ……………………………………………PRIMARY SCHOOL: FROM …………………………….

TO ………………………

**C: PREVIOUS SECONDARY SCHOOL (IF TRANSFER TO THIS SCHOOL)**

NAME OF THE SCHOOL: …………………………………………………………………………………………………………

ADDRESS: …………………………………………………………………………………………………………………………

"I CERTIFY THAT THE ABOVE INFORMATION IS CORRECT TO THE BEST OF MY KNOWLEDGE"

……………………… …………………………………………………………………… ……………………………………

**DATE** **NAME OF STUDENT** **STUDENT SIGNATURE**

**D: (TO BE COPLETED BY FORM COORDINATOR):**

DATE OF ADMISSION TO THIS SCHOOL……………………… DATE OF ADMISSION NUMBER…………………………………

ADMISSION NUMBER …………………………… YEAR ……………. FORM ADMITTED …………………… YEAR ………………………

DATE OF LEAVING SCHOOL………………………………………… HIGHEST FORM REACHED…………………………………………

SIGNATURE OF FORM CO-ORDINATOR …………………………………………… DATE …………………………………………………

SIGNATURE OF THE HEADMISTRESS …………………………………………………… DATE ……………………………………………..

**FORM D**

**OFISI YA WAZIRI MKUU - TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA SIHA**

**SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA KILIMANJARO**

**AHADI YA MZAZI**

Mimi mzazi wa mwanafunzi……………………………………………………kidato cha…………………………………………

Mwaka……………………………ninakiri kukubaliana na sheria ,kanuni kulipa michango ya shule na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule kipindi chote mwanangu atakapokuwa katika Shule ya Sekondari ya Wasichana Kilimanjaro.

MAJINA YA WAZAZI/WALEZI PICHA

1.JINA……………………………………………………………………….

NAMBA YA SIMU…………………………………………………………

UHUSIANO…………………………………………………………………..

SAINI…………………………………………………………………………

TAREHE……………………………………………………………………

2.JINA……………………………………………………………………….

NAMBA YA SIMU…………………………………………………………

UHUSIANO…………………………………………………………………..

SAINI…………………………………………………………………………

TAREHE……………………………………………………………………

3.JINA……………………………………………………………………….

NAMBA YA SIMU…………………………………………………………

UHUSIANO…………………………………………………………………..

SAINI…………………………………………………………………………

TAREHE……………………………………………………………………

**FORM E**

**OFISI YA WAZIRI MKUU - TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA SIHA**

**SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA KILIMANJARO**

## FOMU YA USAJILI WA MWANAFUNZI

1. JINA………………………………… Kidato cha……………………………
2. Tarehe ya kuingia…………………………………………………………..

### 3.UKAMILISHAJI WA MAHITAJI

i. Sare ya shule:Amekamilisha/Bado Anadaiwa…………………………………

ii.Vifaa vya masomo.Amekamilisha/Bado Anadaiwa…………………………

iii.Ream:Amekamilisha……………………………Bado……………………………….

iv.Vifaa vya bwenini kwa matumizi binafsi Amekamilisha/Bado……………………………………

V. **Vifaa vya usafi.**

**1.Fagio la kutolea buibui -01**

**2.Mopper na doo yake-01**

**3.Sabuni ya maji-LT 05**

**4.Slasher/fyekeo-01**

**JINA LA MHASIBU……………………………….SAINI……………………………. TAREHE……………………………….**

**JINA LA MWALIMU WA ZAMU………………………………………. SAINI…………………TAREHE………………….**